

# Sayansi ya siasa

na Dk Elizabeth Baldwin,  
Dk Jennifer Brass,  
Dk Christopher Gore,  
Dk Lauren MacLean,  
Dk Winnie Mitullah  
na Dk Alesha Porisky

## Pointi za mazungumzo

### Maarifa

1. Je, ni sehemu gani ya kaya za Kenya zina uwezo wa kupata umeme?
2. Ni kiasi gani cha umeme huu kinachozalishwa kutoka kwa vyanzo vinavyoweza kurejeshwa?

### Ufahamu

3. Kwa nini Wakenya wengi wana uwezo mdogo wa kutumia umeme, hata kama wana uwezo wa kuupata kinadharia? Je, ni vikwazo gani vikubwa vya matumizi ya umeme zaidi vinavyokabili kaya?
4. Ni zipi baadhi ya faida za upatikanaji wa umeme?
5. Je, upatikanaji wa umeme unaathiri vipi namna Wakenya wanavyoshiriki katika shughuli za kiraia (k.m. mikutano ya jumuiya) na shughuli za kisiasa?

### Uchambuzi

6. Je, unafikiri kaya na wafanyabiashara wa Kenya wanakabiliwa na matatizo gani kutokana na ukosefu wa umeme wa uhakika na kukatika katika mara kwa mara?
7. Ni kwa namna gani, uzoefu wa kibinafsi wa kila mshiriki wa timu umechangia safari yao ya kazi?

### Tathmini

8. Lengo la 7 la Maendeleo Endelevu la Umoja wa Mataifa ni 'kuhakikisha upatikanaji wa nishati nafuu, ya uhakika na endelevu kwa wote ifikapo mwaka 2030'. Je, ni kwa kiasi gani unaamini kuwa haya ni malengo ya ulimwengu yenye kutimizika? Ni vikwazo gani vinavyoweza kuzuia hili kufikiwa katika nchi yako? Ni masuluhisho gani yanaweza kusaidia kupambana na changamoto hizi?

## Shughuli

### Fikiria maisha bila umeme

Orodhesha njia zote ulizotumia (au kunufaika nazo) kutokana na umeme jana. Hii inaweza kujumuisha kuchaji simu yako, kutazama TV, kuwasiliana na marafiki mtandaoni, kuwa ndani ya chumba chenye mwanga wa umeme, kula chakula kilichohifadhiwa kwenye friji na/au kupikwa kwenye jiko la umeme, kusafiri kwa gari la umeme, n.k.

Kwa kila kipengee kwenye orodha yako, zingatia jinsi kingeathiriwa ikiwa ungepitia kukatika kwa umeme kwa masaa kadhaa. Ni kwa namna gani ungefanya ili uweze kuendana na siku yako? Kisha, fikiria ni jinsi gani ingeathiriwa ikiwa huna uwezo wa kupata umeme. Unawezaje kurekebisha shughuli hizi ili kutengeneza vitu visivyotumia umeme? Ni shughuli gani zisingewezekana kabisa bila ya umeme?

Tafakari jinsi maisha yako yangekuwa tofauti ikiwa upatikanaji wako wa umeme sio wa uhakika au haupo kabisa.

### Umeme katika Afrika

Chagua mada inayohusiana na umeme barani Afrika, kama vile viwango tofauti vya upatikanaji wa umeme, changamoto ambazo watu hukabiliana nazo kwa kukosa umeme wa uhakika, au rasilimali za nishati mbadala za Afrika. Tafiti mtandaoni ili kujifunza zaidi kuhusu mada yako na kupata ukweli na takwimu za kuvutia, kisha andaa bango au wasilisho linalovutia ili kushiriki matokeo yako na wanafunzi wenzako.

### Umeme kwa AI

Kuongezeka kwa upatikanaji wa umeme katika nchi zinazoendelea ni muhimu kwa kuhakikisha kwamba kila mtu anapata mahitaji ambayo yanaboresha ubora wa maisha yake, kama vile taa na mawasiliano. Lakini utoaji wa umeme pia ni mada ya mjadala katika nchi zilizoendelea. Kuongezeka kwa akili ude (AI) kunaleta hitaji kubwa la kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme, kwani vituo vya data ambavyo vinaendesha mifumo ya AI vinahitaji kiwango kikubwa cha nishati. Fanya tafiti mtandaoni ili kupata maelezo zaidi kuhusu mahitaji ya nishati ya vituo vya data vya AI, kisha uandae mjadala wa darasa kuhusu mada hii (k.m., kuhusu athari za kimazingira za AI au ikiwa nchi zilizoendelea zinapaswa kuwekeza katika umeme kwenye nchi zinazoendela badala ya katika vituo vyao vya data vya AI).

## Nyenzo zaidi

- Tembelea ukurasa wa timu ya Futurum ili kusoma makala kwa Kiingereza: [www.futurumcareers.com/how-does-access-to-electricity-impact-citizens-in-Kenya](http://www.futurumcareers.com/how-does-access-to-electricity-impact-citizens-in-Kenya)
- Pata maelezo zaidi kuhusu utafiti wa kijamii uliofanywa na mshirika wa timu, Utafiti wa TIFA Kenya: [www.tifaresearch.com](http://www.tifaresearch.com)
- Pata maelezo zaidi kuhusu Lengo la 7 la Maendeleo Endelevu, gundua jinsi unavyoweza kuchangia kulifikia, na upate nyenzo muhimu za elimu: [www.globalgoals.org/goals/7-affordable-and-clean-energy](http://www.globalgoals.org/goals/7-affordable-and-clean-energy)